
Mafundisho
ya Yesu Mlimani
Ufunguo wa maisha
ya kiroho yenye raha
Sehemu za kitabu

Mafundisho ya Yesu Mlimani

Ufunguo wa maisha ya kiroho yenye raha



First Edition in Swahili: October 2021
1ère édition en Swahili: Octobre 2021

Translated from the original German title:
Traduit de l'allemand, titre original:

Die Bergpredigt
Der Weg zu einem erfüllten Leben

The German edition is the work of reference
for all questions regarding the meaning of the contents
Pour toute question se rapportant au sens,
l'édition allemande fait référence

© All Rights Reserved / Tous droits réservés
Gabriele-Verlag Das Wort GmbH

Kristu anazungumza

(Sehemu za kitabu «*Hili ndilo Neno Langu*»)

Mafundisho ya Mlimani ni njia ya kiroho inayoongoza moyoni mwa Mungu, kwenye ukamilifu.

Ninaongoza watu wangu kwenye ufahamu wa ukweli.

«*Heri walio maskini wa roho, maana Ufalme wa Mbinguni ni wao!*»

Neno «*maskini*» halimaanishi ukosefu wa mali». Siyo ukosefu wa mali ndio unaleta raha rohoni bali mshikamano wa kina na Mungu, kwa kutimiza mapenzi yake. Huo ndio utajiri wa kiroho.

Neno «*maskini*» lamaanisha wale wote wasiotafuta kumiliki na kujirundikia mali... Utajiri wao wa ndani ni maisha katika Mungu, kwa manufaa ya Mungu na ya majirani wao. Wanatimiza amri «Omba na tenda kazi».

«*Heri wanaoteswa, kwa maana watafarijiwa*»

Mungu siye mhusika wa mateso ya mwanadamu...

Yeyote anayekubali mateso yake bila kumshtaki jirani yake na ambaye katika mateso yake, anatambua makosa na udhaifu wake, anatubu makosa yake na anaomba msamaha na anasamehe, atapata rehema ya Mungu.

«*Heri wenye upole, maana watarithi nchi.*»

Upole, unyenyekevu, upendo na wema vinaambatana. Mtu anayependa bila kulenga faida ni mpole, myenyekevu na mwema pia. Amejaa hekima na nguvu.

«*Heri wenye njaa na kiu ya haki, kwa sababu wao watashibishwa.*»

Tazama, Mimi, Mkombozi wako, Mimi ni ukweli ndani mwako. Kwa hiyo Mimi ni ndani mwako Njia, Ukweli na Uzima.

Tambua kuwa hakuna mtu angepashwa kuhisi njaa na kiu ya haki. Fanya hatua ya

kwanza kwenye Ufalme wa upendo kwa kuanza kuwa na kaki kwako wewe mwenye. Jizoeze kufikiria na kuishi vema, hatua kwa hatua utageuka mtu wa haki atakayeleta haki ya Mungu katika ulimwengu huu...

«*Heri wenye rehema, maana watapata rehema.*»

Watu wote wanaojitahidi kukuza rehema watapokea rehema na kusaidia wale ambao wangali bado kwenye njia ya rehema.

«*Heri wenye moyo safi, maana wao watamuona Mungu.*»

Watamuona Mungu kwa sababu wamemfanana Baba wa mbinguni. Upole na unyenyekevu hutiririka toka moyo safi ambao unajitoa kwa Mungu tu.

«*Heri wenye kuleta amani, maana wataitwa wana wa Mungu.*»

Maana ya maneno hayo ni haya: Heri wenye kuishi katika amani. Wataleta amani ya kweli duniani kwa sababu wao wenyewe wamegeuka wapatanishi. Kidhamiri wao ni wana wa Mungu.

«Heri wale wanaoteswa kwa sababu ya haki, maana Ufalme wa Mungu ni wao.»

Tambueni kwamba wale waliofuata nyayo zangu hawakutambulika na watu wanaotegemea ulimwengu huu, kwa sababu pia walinidharau wakati nilipokuwa katikaYesu. Katika nyakati zote, wale waliofuata kwa kweli mfano wa Mnazareti walilazimishwa kuvumilia na kupitia mateso mengi.

«Jihadharini nyinyi matajiri! Kwa sababu tayari mmepokea faraja yenu katika uzima huu.»

Mtu tajiri anayemiliki mali ya ulimwengu huu, aliye na dhamiri kwamba utajiri wake ni zawadi ambayo Mungu anampa ili autumie kwa manufaa ya ulimwengu wote na ya wote, na anayeutumia kufuatana na Sheria ya Mungu na kwa faida ya watu wote, anatimiza Sheria ya usawa, uhuru, umoja na undugu.

Hayo inawezesha kujitokeza hatua kwa hatua kwa usawa, kujitokeza kwa tabaka la kati la kiwango cha juu kwa wale walio tayari kutekeleza bila faida Kanuni «omba na fanya kazi».

«Jihadharini Nyinyi mlioshiba, kwani mtakumbwa na njaa.»

Mtu tajiri anayeshiba, na anayejaza tu maghala yake mwenyewe, ana moyo usio na ubinadamu.

«Jihadharini nyinyi mnaocheka leo, kwani kesho mtasikitika na kulia.»

Yule anayemuadhibu na kumhukumu mwenziwe, anayemchekelea, anayemdhihaki na kumsingizia, ananiadhibu, kunihukumu na kunisingizia Mimi Kristu.

Tambueni kwamba mtu yeyote anayemtendea vibaya mdogo sana wa ndugu Zangu, anafanya dhambi dhidi ya sheria ya Uzima, atateswa siku moja kwa ajili ya hayo.

«Jihadharini ikiwa watu wote wanasema mambo mazuri kuhusu nyinyi, kwa kuwa baba zenu walitenda hivyo kwa manabii wa uwongo.»

Wakati unapomsifu mwenziwe ili uonekane mwema na upate shukrani yake, wewe ni kama tapeli anayelipa pesa bandia kwa kujipatia faida.

Miongoni mwa manabii wa uwongo, mna wale ambao waliohubiri Injili ya upendo bila kuitimiza maishani mwao.

Leo, kwa wakati huu wa machafuko makubwa na wa mabadiliko ya ulimwengu wa zamani wa dhambi kuingia kwenye Enzi Mpya, enzi ya nuru, wenye haki wataweka bayana dhuluma na kuidhihirisha ili wale waliyoifanya watubu na wajirekebishe.

Mimi ni nuru ya ulimwengu.

Hata leo tena, wamilele anajitahidi kuwaelekeza wanae wanadamu wote na nafsi zote kwenye moyo wake, kwenye Sheria ya upendo wa milele kabla mavuno – yaani madhara ya matendo maovu waliofanya – haijawaathiri. Kupitia Mimi, Kristu, Wamilele anawaelekeza wajitambue wao wenyewe.

Anawapa nguvu ya kuacha dhambi na makosa wanayoyatambua.

Jueni kwamba katika Sheria ya milele, hakuna udikteta. Mungu, Wamilele, amewapa wanae wote uamzi huru.

Madhehebu kadhaa yanayojidai kuwa ya kikristu hulazimisha waumini wao kubatizwa kwa maji. Huo ni ukosefu wa heshima

dhidi ya uamzi huru wa mtu, ni ukristu wa kulazimishwa.

Ni kwa kujitenga tu kwa hiari na kanuni za kidini, na misimamo migumu, maabudu ya kulazimishwa, na pia kwa kutupilia mbali picha tunazojifanyia kuhusu Mungu, ndipo inawezekana kuelekezwa hatua kwa hatua moyoni, kwenye utu halisi.

Wakati maneno yenye maana karibu na haya yalipotamkwa: «Yote yametimia», cheche za nuru ya ukombozi zikapenya ndani ya nafsi zote zenye dhambi na zilizoshushwa. Hivi ndivyo nikawa na ndivyo ningali bado Mkombozi wa wanadamu wote na wa nafsi zote.

Nilitenda kama Kristu wa Mungu na ninaendelea kutenda hivyo.

Amri Kumi zilizotolewa na Mungu kwa wanae wanadamu kupitia Musa ni dondoo za Sheria ya milele ya Uzima na ya upendo. Yule anayetenda kinyume cha Amri hizo, na kuzifundisha bila kuzishika ni mdanganyifu. Anatenda dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu. Ni dhambi kubwa zaidi.

Tambueni kwamba haitoshi tu kuamini Sheria ya Uzima. Kuamini Uzima na utekelezaji wa Sheria ya Uzima ndivyo vinavyomtenga mwanadamu na pia nafsi yake na tendo la kuzaliwa upya duniani baada ya kifo.

«...*Jipatanishe na ndugu yako.*»

Amri ya kusamehe na kuomba msamaha itazidi kudumu hadi muda ambapo jambo lote lililo kinyume na Sheria ya milele litakapolipizwa na kurekebishwa.

Ndani ya jambo mbaya lote mnapatikana pia mazuri yaani Mungu, Sheria ya milele. Wakati mtu anatambua makosa na dhambi zake na kuzitubu, nguvu nzuri ndani mwake hutenda kazi...

Ndiyo sababu yaliyo ya Mungu yanaweza kutenda kazi ndani ya maovu, mara tu mtu anapoomba msamaha kwa moyo wote, akisamehe na akiacha kutenda dhambi.

Ikiwa unatumia maneno iliyo kinyume na Sheria kwa kushtaki, kutusi au kwa kusema maneno mabaya dhidi ya jirani yako, ebu! nenda ukamuombe msamaha.

Akikusamehe, basi Baba wa mbinguni na wa milele ndani Mwangu, Kristu,

anakusamehe pia. Ila ikiwa jirani yako anakataa kukusamehe, Baba wa mbinguni na wa milele ndani Mwangu, Kristu, hawezi pia kukusamehe...

«Jipatanishe haraka iwezekanavyo na adui yako, wakati mungali bado pamoja...»

Usichelewe kurekebisha uovu uliomtendea jirani yako!

Fanya hivyo hima wakati bado mnaishi pamoja duniani.

Tambua kwamba, kabla ya madhara kumpata mtu, Roho wa Uzima aliye pia Uzima wa nafsi, malaika mlinzi wake au majirani zake humuonya. Maonyo toka Roho ni hisia safi sana zinazotiririka toka nafsi au zinazotolewa na malaika mlinzi kwenye jumla ya hisi au mawazo yake. Hisi na mawazo vinamuonya arekebishe namna yake ya kufikiri au akosoe jambo mbovu lile alilofanya.

«Ila Mimi ninawaambieni..: Pendeni adui zenu, watendeeni mema wanaowachukia.»

Kila mmoja angepashwa kuwachukua majirani wake wote kama ndugu au dada. Mgepashwa vilevile kuchukua kama majirani

wenu wale wanaonekana kuwa «maadui» wenu, na kuwapenda bila kulenga faida.

Anayejiita adui anaweza kuwa kwako kioo kizuri kinachokuwezesha kujitambua mwenyewe ; hakika, ikiwa jambo Fulani kuhusu jirani yako linakukasiriha, hayo yana maana kwamba una jambo hilo au la kukifanana na hilo ndani mwako.

«Kwa sababu ukiwapenda wale wanaokupenda, utakuwa na sifa njema ipi ?»

Mkubali na kumpa nafasi moyoni jirani yako, hata kama mwenyewe hakupendi, hakusaidii, na anakudharau kwa kutokusalimu. Wewe, mpende ! Wewe, msaidie bure na msalimu tu hata katika fikra, ikiwa hataki umsalimu kwa maneno.

Penda bila kutegemea faida, kama jua litoleavyo nuru Ulimwengu na heshimu watu wote na aina zote za viumbe.

Usijipendekeze kwa majirani wako. Usifanye tofauti kati ya watu kama wafanyavyo watu wanaotembelea na kukubali tu watu wanaoafikiana nao kifikra na kimwenendo ila wanaolaumu watu wanaofikiri na kutenda tofauti nao.

«Na ukitamani sana kitu kinachoweza kusababishia wenzio mateso na dhiki, Kiondoe moyoni mwako...

Kwa hiyo muwe watakatifu kama Baba yenu wa Mbinguni alivyo mtakatifu.»

Wakati unapokumbwa na mateso na shida, usiwashtaki wengine kuwa wausika. Ni wewe ndiye mhusika. Ni wewe mhusika, bali si wao. Mateso hayo hutokana na kile ulichopanda nafsini mwako na sasa kinachojidhihirisha kama mavuno katika mwili na maisha yako. Mimi, Kristu, Mkombozi wako, Ni Mimi peke yangu ndiye ninaweza kukuokoa toka hali hiyo ikiwa unatubu na kutorudilia uovu huo au unaofanana nao. Utaondolewa dhambi nafsini mwako na utafanikiwa.

«Unapotoa sadaka, usiruhusu mkono wako wa kushoto ujue kile mkono wako wa kulia unachofanya, hivyo zawadi yako itabaki imefichwa.»

Yeyote anayemtendea wema mwenziwe kusudi huyo amshukuru na kumsifu kwa matendo yake mema, mtu huyo hatendi kwa ajili ya jirani wake bali kwa manufaa yake mwenyewe.

«Wakati Unapoomba, ingia chumbani mwako...»

Unapoomba, ingia kwenye chumba chako tulivu na elekeza makini yote ndani mwako, kwa kuwa Roho wa Baba ambaye wewe ni hekalu lake, anakaa ndani mwako.

Tambueni kwamba kadiri mtu alivyojitumbukiza katika ukweli wa Mungu, ndivyo hana tena haja ya maneno kwa kujieleza, ni hivyo pia wakati wa maombi.

Maombi yake ni mafupi lakini yenye nguvu kwa sababu maneno yake inadhihirisha nguvu anazozihisi.

«...msinung'unike kama wale wasio na tumaini.»

Msiomboleze wafu wenu !

Uhai wa muda katika mwili wa mwanadamu, siyo Uzima wa nafsi. Nafsi iliingia tu mwilini kwa muda mfupi kwa ajili ya matengenezo na malipo ya deni, katika uzima huu wa muda, ya uovu ambao nafsi ilijitwika wakati wa maisha mengine ya awali duniani.

Jueni kwamba kwa nafsi yenye nuru, kujitenga na mwili ni faida.

Nafsi huhisi furaha na mateso ya ndugu zake. Nafsi safi zilizoacha mwili wa dunia hujihisi zimeunganishwa na Mimi Kristu, na zote ambazo bado zimezaliwa upya duniani. Furaha ambayo nafsi huhisi inapotambua kwamba wenziwe wanamjali kwa upendo huijaza nguvu.

Tazama, sala za upendo usiolenga faida huipa nafsi nguvu katika njia yake ya kwenda kwa Mungu. Inahisi umoja uliomo ndani ya sala hizo na inapata nguvu za ziada kutoka sala hizo.

Tambueni kwamba ni upendo na umoja peke yao ndivyo njia ya kupitia kwa kuelekea kwenye uzima wa juu vikitumiwa na wamoja kwa wengine, na nafsi kama vile mtu ambamo nafsi ilimozaliwa upya.

«*Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili.*»

Duniani, kama mwanadamu, au katika mazingira ya utakaso kama nafsi, siku moja kila mmoja ataombwa kuamua: kumtumikia Mungu au shetani, kumpenda Mungu au kumpinga. Hakuna uhusiano kati ya mambo

hayo mawili : mtu huwa upande wa Mungu au ule wa shetani.

«Usijali mateso ya kesho...»

Yeyote anayetimiza mapenzi ya Mungu ni mratibu mwema.

Fanya mpangilo wa kila siku na uipangilie vema! Jipe pia muda wa kutafakari ambapo unaweza kupata utulivu wa ndani wa kutafakari mara na mara kuhusu maisha yako na kuhusu kile ulichokipangilia. Ikiwa mpangilio bora wa siku umewekwa mikononi mwa Mungu, Mungu ataujaza pia na mapenzi yake.

Ni mtu yule tu asiyejikabidhi kwa Mungu na anayeacha siku zipite bila ya kuzitumia kwa manufaa yake, ndiye aliye na wasiwasi kuhusu maisha ya siku za usoni.

«Msihukumu, ili msihukumiwe.»

Tambua kwamba, mawazo, maneno na matendo yako mabaya ndiyo waamzi wako.

Mtapimwa «kwa kipimo mnachokitumia» iwe kwa mawazo, kwa maneno aidha kwa matendo.

«Kwanini unaona jani ndogo lililo ndani ya jicho la ndugu yako na huoni boriti iliyo ndani ya jicho lako ? »

Anayemsengenya jirani wake, asiyemthamini na kumshuhudia uongo, hushuhudia kwamba hatambui makosa yake mwenyewe.

Ni kwa matunda yao ndiyo mtawatambua! Kupitia mwenendo wake, kila mtu anaonyesha mwenyewe kuwa yeye ni nani. Mtu anayekasirikia wenziwe na kuwadharau, anaonyesha hivyo hali yake halisi. Yeyote anayeanza kwanza kujiweka huru toka makosa yake mwenyewe, anaweza pia kumsaidia jirani yake.

Bali, yule anayesimulia kwa dharau kuhusu makosa ya mwenziwe-na kwa kufanya hivyo, haoni boriti katika jicho lake mwenyewe, ni mnafiki.

«Chochote unachotaka wengine wakutendee, ukiwatendee wao kwanza...»
Ni kinyume cha Amri kuwa na mtazamo wa matarajio unaomlazimisha jirani kutenda, kujieleza au kuenenda ingawaje hakuwa tayari kufanya hivyo kwa hiari yake mwenyewe.

Ikiwa umetambua matarajio unayo kwa jirani yako, hebu jirekebishe upesi sana na timiza mwenyewe kile unachotaka akutimizie.

Kile usichotaka wakutendee, usikitendee mtu yeyote kwa sababu kila kitu kinachotokana nawe kitakurudilia. Ndiyo sababu chunguza fikra na maneno yako.

«*...Ninamlinganisha yule anayesikia neno langu na kulitimiza na mtu mwenye busara aliyejenga vema nyumba yake juu ya mwamba.*»

Sehemu toka kitabu:

«Hili ni Neno langu. Alfa na Omega. Injili ya Yesu. Ufunuo wa Kristu wa Mungu unaojulikana na wakristu wa kweli wa ulimwenguni pote.»

Vijitabu vitolewavyo bila malipo

- Kumpata Mungu! Wapi? Na Vipi?
- Usikate tamaa! Stahimili!
- Mungu ndani mwetu
- Mnaishi milele. Hakuna mauti





Yesu wa Nazareti alikuwa nani?

Utoto na ujana wake

Kitabuni humu mmekusanywa vifungu tofauti vya ufunuo wa Kristo, ambamo mwenyewe anaeleza hadithi ya maisha yake duniani katika Yesu wa Nazareti, kwa upekee ujana na utoto wake. *(Kurasa 48)*



Jifunze kuomba

Katika sala ya kweli, unapata maarifa ya Mungu. Sala halisi humfanya mtu awe mwenye raha.

Ila, sala halisi, huhitaji mafunzo, kwa kuwa, sala halisi, tunayoifanya ndani mwetu wenyewe, ni mazungumzo na Mungu. *(Kurasa 56)*



Amri Kumi za Mungu zilizotolewa kupitia Musa

na kufafanuliwa katika usemi wa siku hizi, ni mashauri ya uzima yenye thamani kubwa inayomwezesha mtu kupata Amani ya roho, uhuru na kumsaidia kumkaribia hauta kwa hatua Mungu, Roho huru aliye ndani mwetu na ndani ya viumbe vyote. *(Kurasa 44)*

Vitabu hivi vinapatikana pia katika lugha ya kiingereza, kifaransa na nyingine nyingi pia

Infos at WhatsApp/Viber in English: +49 151 1883 8742
Infos par WhatsApp en français: +49 159 08 45 45 05
Gabriele-publishing.com



Gabriele Publishing
The Word

Max-Braun-Straße 2 • 97828 Marktheidenfed • Germany

www.gabriele-publishing.com